

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA PILI

02 FEBRUARI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA PILI – TAREHE 02 FEBRUARI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

1. **MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini agizo la Mheshimiwa Rais la kuboresha Stendi ya Bweri Musoma Mjini litatekelezwa.

2. **MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ziba Wilayani Igunga; aliyoitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

3. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha kipengele cha *moving expenses* kilichotolewa ili Watumishi walipwe fedha za nauli wakati wakisubiri kulipwa mafao mengine.

WIZARA YA MAJI:

4. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza dhamira yake ya kuwatua Wanawake ndoo kichwani kwa kusogeza huduma za maji safi na salama karibu na makazi yao katika Jimbo la Mwibara.

5. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji kwa Wananchi wa Vijiji vya Kata za Imasela, Ilola, Lyamidati, Lyabukande na Nyida ambazo zipo ndani ya Km 12 kutoka katika mtambo wa maji wa Ziwa Victoria.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

6. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua Uwanja wa Ndege wa Kigoma ili Ndege kubwa ziweze kutua.

**7. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA
(MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza upembuzi yakinifu wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Manyoni *East* – Heka – Isseke – Sanza hadi Dodoma.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**8. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-


Je, Serikali haioni umuhimu wa kukutana na Wafanyabiashara na kutafuta namna bora ya kuwa na utaratibu wa ukadiriaji kodi wenye usawa na unaozingatia mabadiliko ya biashara ili kulinda mahitaji ya Wafanyabiashara wa ndani.

9. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Utoaji wa leseni kwa biashara ndogo za maduka katika Manispaa ya Kinondoni umekuwa na changamoto kutokana na Wafanyabiashara hao kutokuwa na *Tax Clearance* kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA):-

Je, ni kwa nini Serikali isiagize TRA kwenda mitaani na kubaini biashara hizo na kuzisajili kwa lengo la kurahisisha utoaji wa *Tax Clearance* ili leseni ziweze kutolewa.



WIZARA YA AFYA:



10. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Wodi za Wagonjwa wenye matatizo ya Ubongo na Akili katika Hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala.

**11. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa Madaktari Bingwa na Vifaa Tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete Mkoani Tabora.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**12. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia Wavuvi elimu ya uelewa kuhusu madhara ya uvuvi haramu ili wasifanye aina hiyo ya uvuvi na kuharibu mazingira ya Maziwa na Bahari nchini.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

13. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,
Sanaa na Michezo:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kutoa ajira rasmi
na zisizo rasmi kupitia Tasnia ya Sanaa.

WIZARA YA NISHATI:

14. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

- (a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere;
- (b) Je, kwa nini Mkandarasi ameshindwa kujaza maji kwenye Bwawa kufikia tarehe 15 Novemba, 2021 kama ilivyokuwa imekubalika;

(c) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kutokana na ucheleweshwaji huo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

15. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni upi mgawanyo wa Vitabu 812 vya nukta nundu vilivyotolewa katika mpango wa fedha za mapambano dhidi ya UVIKO-19.

**DODOMA
02 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**